

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA KUMI NA NANE

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO  
*(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)*

31 JANUARI, 2015

## **MKUTANO WA KUMI NA NANE**

### **YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO (SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS - FIFTY SITTING) TAREHE 31 JANUARI, 2015**

#### **I. DUA**

Dua ilisomwa na kikao kilanza saa 3.00 asubuhi kikiongozwa na Mhe. Anne S. Makinda, Mb (Spika wa Bunge).

#### **MAKATIBU MEZANI:**

1. Ndg. Charles Mloka
2. Ndg. Lawrence Makigi
3. Ndg. Lina Kitosi

#### **II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:**

Mhe. Esther Bulaya , (Mb), kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira aliwasilisha Mezani Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira katika Kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

Mhe. Said Mkumba, (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji aliwasilisha Mezani Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji katika Kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

### **III. HOJA ZA KAMATI:**

Mhe. Peter Serukamba, (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Miundombinu pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

Mhe. Richard M. Ndassa, (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini; kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

Mhe. Spika aliwahoji Wabunge kuhusu kupunguza Muda wa kuchangia kutoka dakika 15 hadi dakika 10 ili kutoa fursa kwa Wabunge wengi kuchangia. Wabunge walifiki muda wa kuchangia kuwa dakika 10 badala ya dakika 15.

### **ORODHA YA WACHANGIAJI:**

1. Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile, Mb
2. Mhe. Said Arfi, Mb
3. Mhe. Moses Machali, Mb
4. Mhe. Riziki Lulida, Mb
5. Mhe. Martha M. Mlata, Mb
6. Mhe. Selemani Kakoso, Mb
7. Mhe. Shamis Haroub Mohamed, Mb

8. Mhe. Omari Nundu, Mb
9. Mhe. Ali Kessy, Mb
10. Mhe. Abdul J. Marombwa, Mb
11. Mhe. Rebecca Mngodo, Mb
12. Mhe. Christopher Ole-Sendeka, Mb
13. Mhe. Rajab Mbarouk Mohamed, Mb
14. Mhe. Selemani Jaffo, Mb
15. Mhe. Jitu Sonni, Mb

Baada ya Wabunge kuchangia Mhe. Spika aliwaita Mawaziri Wafuatao ili kujibu hoja zilizotolewa na Wabunge wakati wakichangia Hoja za Taarifa za Kamati za Kisikta.

1. Mhe. Samwel J. Sitta (Mb) – Waziri wa Uchukuzi
2. Mhe. Greyson Lwenge (Mb) – Naibu Waziri wa Ujenzi
3. Mhe. Januari Makamba (Mb) – Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.
4. Mhe. Charles Mwijage (Mb) – Naibu Waziri wa Nishati na Madini.
5. Mhe. Saada S, Mkuya (Mb) – Waziri wa Fedha

Mhe. Spika alimuita Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ili waweze kuhitimisha hoja za Kamati zao.

Mhe. Spika aliwaarifu Wabunge kuwa Maelezo kuhusu Sheria ya Tax Administration yatatolewa siku ya Jumatatu.

#### **IV. KUAHIRISHA BUNGE:**

Mhe. Spika alahirisha Bunge saa 7.40 mchana hadi siku ya Jumatatu.

**DODOMA**  
**31 JANUARI, 2015**

**DKT. T.D. KASHILILAH**  
**KATIBU WA BUNGE**